



EMBASSY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA PARIS

TELEGRAPH-ADDRESS: TANZANREP PARIS
TELEPHONE: 01 53 70 63 66
Fax: 01 47 55 05 46
E-mail: ambtanzanie@wanadoo.fr.
Website: www.tanzaniaembassy.fr

7 TER RUE LEONARD DE VINCI
75116 PARIS.
FRANCE

ALL Official correspondence must be addressed
to Her Excellency The Ambassador

Please quote Ref. No. TZP/P.200/2

Paris, 02/03/2015

PASI MPYA / NEW PASSPORTS

Pasipoti za sasa ni kwa matumizi ya mtu mmoja tu, watoto wanatakiwa kuwa na pasipoti na watafuata taratibu zote zinazohitajika za utoaji wa pasipoti mpya.

Fomu za maombi zisomwe na zijazwe kwa makini na sahihi itatiwa mbele ya afisa wa Ubalози.

Hakikisha unapiga picha ambazo nyuma yake zinaonyesha rangi ya maji bahari (skyblue background). Huduma ya picha iko katika studio karibu na Ubalози kwa gharama ya € 6. Idadi ya picha zinazohitajika ni 5.

NB: Kuepuka usumbufu tafadhali fanya miadi (appointment) na Ubalози kabla ya kuja.

Utaratibu wa kutoa pasipoti mpya utakuwa kama ifuatavyo:

(A) Maombi:

- Mwombaji atachukua fomu za kuomba pasipoti (CT 5A1) kutoka hapa ubalozini.
- Mwombaji anatakiwa awasiliane na Ubalози ili apewe miadi (appointment) ya kurejesha fomu hizo pamoja na viambatanisho vyake kamili na kukamilisha kuchukua alama za vidole na kuweka sahihi mbele ya afisa wa pasipoti.
- Kwa waombaji ambao wanaishi kwenye miji nje ya Paris inashauriwa wawasiliane na afisa anayehusika ili awape miadi (appointment) ya kuja Paris na kushughulikiwa siku atakayopangiwa na afisa husika. Tafadhali zingatia kuwa na mahitaji yote yanayotakiwa ili kuepuka usumbufu.

(B) Kujaza na Kurudisha Fomu

- Fomu inatolewa baada ya kulipa ada ya 10 Euro. Fomu hizi zina "original serial numbers" hivyo hazitolewi nakala na kuzigawa kwa mtu mwingine.
- Fomu zijazwe kwa makini na sahihi itajazwa baadaye mbele ya afisa wa ubalozi. Mwombaji akikosea kujaza fomu atatakiwa kulipia fomu nyingine kwa Euro 10 (kumi).
- Maombi yote yatajazwa kwa HERUFI KUBWA NA KWA WINO MWEUSI.
- Wakati wa kurejesha fomu hiyo mwombaji atachukuliwa alama za vidole na afisa Ubalozzi husika na kuweka saini yake katika fomu mbele ya Afisa anayeshughulikia pasipoti, kwa kutumia kalamu maalum.

(C) Viambatanisho

- Mwombaji atahitajika kuleta picha tano (5) 'passport size' (zenye urefu wa 4.5cm na upana 4cm) ambazo nyuma yake zinaonyesha rangi ya maji bahari (skyblue background).
- Kivuli cha Pasipoti yake ya Tanzania inayoonyesha nakala ya mwanzo na ya mwisho inayoonyesha Dossier Number (DN).
- Kwa mwombaji wa mara ya kwanza, kivuli cha cheti halisi cha kuzaliwa kiambatanishwe.
- Kivuli cha kadi ya ukazi (titre de séjour)
- Ada ya pasipoti ni 50 Euro

Tafadhali hakikisha viambatisho vyote vinatolewa kopi kabla ya kuja Ubalozini. Ubalozzi hautatoa kopi kwa viambatisho vya muombaji.

(E) Utoaji Pasi

- Maombi yatatumwa Makao Makuu ya Uhamiaji Dar es Salaam. Pasipoti zitakapokuwa tayari waombaji wataarifiwa ili waje kuzichukua ubalozini.
- Wakati wa kuchukua pasi mpya pasi ya zamani itawekwa alama ya kufutwa uhalali wake.

Atakayepata ujumbe huu amwambie na mwenzie!!!!!!!!!!

KARIBUNI !

Robert Mahundi
Kny: BALOZI